JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



# MWONGOZO WA UTEKELEZAJI WA MKAKATI WA TAIFA WA ELIMU JUMUISHI 2022-2026

Oktoba, 2022

Mwongozo huu umeandaliwa na:

**OFISI YA RAIS**

Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa



# DIBAJI

Ofisi ya Rais - TAMISEMI ina jukumu la kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa Sera, Mikakati na Sheria za Elimu inayotolewa na Serikali ili kuimarisha utoaji wa Elimu nchini katika mazingira jumuishi. Katika kutekeleza jukumu hili, imebaini kuwepo kwa utofauti mkubwa kweye utekelezaji wa elimu jumuishi kati ya shule moja na shule nyingine, Halmashauri moja na nyingine, hata Mkoa mmoja na mwingine nchini. Ili kuondoa tofauti hiyo, OR- TAMISEMI iliunda kikosi kazi cha Wataalamu Wabobezi wa Elimu Maalumu/ Jumuishi kwa lengo la kuandaa Mwongozo huu ili uwe nyezo stahiki katika utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Elimu Jumuishi uliopo.

Mwongozo umebainisha changamoto mbalimbali zinazoathiri ufanisi wa utoaji wa elimu katika mazingira jumuishi. Aidha, umechambua kwa undani hali halisi ilivyo na kuonesha fursa zilizopo, utatuzi wa changamoto pamoja na viashiria vya upimaji wa mafanikio ya utekelezaji wake. Mwongozo huu unalenga kuweka taratibu za utekelezaji katika ngazi mbalimbali za wasimamizi na watekelezaji wa elimu na kutoa fursa kwa wadau mbalimbali kushirikiana na serikali katika kutekeleza utoaji wa elimu katika mazingira jumuishi.

Vilevile, unalenga kuainisha namna ya utekelezaji wa maeneo matano ya utekelezaji kama yalivyobainishwa kwenye Mkakati wa Taifa wa Elimu Jumuishi. Mwongozo huu umetafsiri na kuainisha majukumu mbalimbali ya utekelezaji katika maeneo mahususi ya ki-sera ambayo ni pamoja na; 1. Sera ya elimu, Sheria na miongozo mbalimbali ya Serikali, 2. Uboreshaji wa mazingira ya utoaji wa

elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum, 3. Uimarishaji wa utamaduni jumuishi wenye kuhimiza usawa katika jamii, 4. Uimarishaji wa uhusiano na ushirikiano na wadau wa elimu, na 5. Ufuatiliaji na tathmini ya utoaji wa elimu katika mazingira jumuishi.

Matokeo tarajiwa ya utekelezaji ni kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu wanaosajiliwa na kukamilisha mzunguko wa elimumsingi kwa mafanikio; na kuongeza ari ya ujifunzaji unaojenga umahiri. Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta watashirikiana katika utekelezaji wa Mwongozo. Hivyo, ni rai yangu kwa kila msimamizi wa elimu kuutumia katika kuleta matokeo tarajiwa.



Prof. Riziki S. Shemdoe
**KATIBU MKUU – OR TAMISEMI**




# SHUKURANI

Utekelezaji wa elimu jumuishi nchini umepitia katika hatua mbalimbali za mafanikio na changamoto zilizopelekea kucheleweshwa kwa upatikanaji wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu – hususani wanafunzi wenye ulemavu. Mwongozo huu utakaotumika kama nyenzo muhimu ya utekelezaji wa elimu jumuishi nchini umetoa maelekezo ya namna ya bora ya kuwezesha utoaji wa elimu katika mazingira jumuishi kwa kuzingatia maelekezo ya Mkakati wa Taifa wa Elimu Jumuishi 2022/26.

Mwongozo huu umeandaliwa na wataalamu wabobezi wa Elimu Maalumu/Jumuishi kutoka Kurugenzi ya Elimu Maalumu – Ofisi ya Rais TAMISEMI, Sekta za Elimu na Asasi za Kiraia.

Shukrani za pekee zimwendee Ndugu Geni J. Migeha (Mkurugenzi Msaidizi Elimu Maalumu, Elimu ya Watu Wazima, Elimu Nje ya Mfumo Rasmi na Elimu kwa Michezo) kwa kusimamia kazi hii, Mwenyekiti wa jopo Dkt. Ildephonce Mkama (Mhadhiri – AMUCTA na Mshauri Mtaalamu wa Elimu Jumuishi – Leonard Cheshire, TO51), Mratibu wa uandaaji wa Mwongozo Ndugu Anna J. Mark (Afisa OR-TAMISEMI), Ndugu Benjamin L. Kihwele (Sense International Tanzania, TO51), Ndugu Lugarata Ng'weshemi, (Afisa OR-TAMISEMI), Ndugu Adam Mkaka (ADD International - Tanzania, TO51), Ndugu Yohanis Kilave (AMUCTA), Ndugu Xavery Haule (Patandi TC), Ndugu Ibrahim Suleiman (Shule ya Msingi Furaha – Tabora) na Ndugu Hildergade Mehrab (Child Support Tanzania).

Mwisho, shukrani ziende kwa Ndugu Ephraim A. Simbeye (Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Elimu), Ndugu Hadija A. Mcheka (Mkurugenzi Msaidizi Elimu Sekondari), Ndugu Sussan S. Nusu (Mkurugenzi Msaidizi Elimu ya Awali na Msingi), ambao

waliratibu na kusimamia shughuli za jopo la wataalamu katika kuandaa kitabu hiki kuanzia hatua ya awali hadi kukamilika kwake. Ni matarajio ya serikali kuwa Mwongozo huu utakuwa ni mwanzo mpya wa utekelezaji wa Elimu Jumuishi kwa ufanisi nchini.



DKT. Charles E. Msonde
**Naibu Katibu Mkuu (Elimu)**

# VIFUPISHO VYA MANENO

| | |
|---|---|
| **OR-TAMISEMI** | Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| **WyEST** | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia |
| **AZAKI** | Asasi za Kiraia |
| **AZASE** | Asasi Zisizo za Kiserikali |
| **NECTA/BAMITA** | Baraza la Mitihani Tanzania |
| **TET** | Taasisi ya Elimu Tanzania |
| **MSM** | Mamlaka za Serikali za Mitaa |

# MAANA ZA ISTILAHI

| | |
|---|---|
| **Elimu Jumushi** | Kulingana na Mkakati wa Taifa wa Elimu Jumuishi 2022 - 2026 elimu jumuishi ni mchakato wa kuongeza ushirikishwaji katika ujifunzaji kwa watoto wote ikiwani pamoja na wenye mahitaji maalumu ili waweze kujifunza bila vikwazo |
| **Shule Jumuishi** | Kulingana na Mwongozo huu shule jumuishi ni shule ambazo mifumo yake ina mazingira rafiki kwa wanafunzi wote bila kubagua wenye mahitaji maalumu |
| **Jamii Jumuishi** | Ni jumuiya ambayo kila mtu pasi kujali tofauti zake za kimaumbile, kijinsia na kiuwezo anashirikishwa katika shughuli mbalimbali za kijamii na kimaendeleo |
| **Wadau wa maendeleo** | Ni watu au taasisi ambazo ziko nje ya mfumo wa serikali zinazochangia maendeleo ya serikali kwa namna moja au nyingine |
| **Utamaduni Jumuishi** | Ni mtindo wa maisha ya jamii fulani yenye kukubali utofauti wa uwezo, jinsia, maumbile, tabia au hali ya ulemavu katika mfumo wa maisha |

# YALIYOMO

**DIBAJI** .......... I

**SHUKURANI** .......... III

**VIFUPISHO VYA MANENO** .......... V

**MAANA ZA ISTILAHI** .......... VI

**SURA YA KWANZA**

**MWELEKEO WA ELIMU JUMUISHI NCHINI** .......... 1

1.1 Utangulizi .......... 1
1.2 Usuli .......... 1
1.3 Malengo ya Mwongozo .......... 1
1.4 Umuhimu wa Mwongozo .......... 2
1.5 Matarajio ya mwongozo .......... 2
1.6 Hitimisho .......... 2

**SURA YA PILI**

**DHANA YA ELIMU JUMUISHI** .......... 3

2.1 Utangulizi .......... 3
2.4 Chimbuko la elimu jumuishi nchini Tanzania .......... 4
2.5 Makundi stahiki ya elimu jumuishi .......... 4
2.6 Changamoto za utekelezaji wa elimu jumuishi .......... 5
2.7 Hitimisho .......... 6

**SURA YA TATU**

**MAENEO YA UTEKELEZAJI** .......... 7

3.1 Utangulizi .......... 7
3.2 Maeneo ya Utekelezaji .......... 7
3.2.1 Kutafsiri kwa vitendo Sera, Sheria, Miongozo, Nyaraka na Matamko ya elimu ili kutekeleza elimu jumuishi nchini .......... 7
MAJUKUMU .......... 7

3.2.1.1 Ofisi ya Rais TAMISEMI ........ 8
3.2.1.2 Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa ........ 8
3.2.1.3 Mkurugenzi wa Halmshauri ........ 9
3.2.1.4 Ofisi ya Kata ........ 9
3.2.1.5 Shule ........ 10
3.2.1.5.1 Kamati na Bodi za Shule ........ 10
3.2.1.5.2 Mkuu wa Shule ........ 10
3.2.1.5.3 Mwalimu ........ 10
3.2.2 Utoaji wa elimu katika mazingira jumuishi ........ 10
MAJUKUMU ........ 12
3.2.2.1 Ofisi ya Rais TAMISEMI ........ 12
3.2.2.2 Ofisi ya katibu Tawala wa Mkoa ........ 12
3.2.2.3 Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ........ 13
3.2.2.4 Ofisi ya Kata ........ 13
3.2.2.5 Shule ........ 14
3.2.2.5.1 Kamati na Bodi za Shule ........ 14
3.2.2.5.2 Mkuu wa Shule ........ 14
3.2.2.5.3 Mwalimu ........ 15
3.2.2.5.4 Msaidizi wa Mwalimu ........ 17
3.3 Hitimisho ........ 17

**SURA YA NNE**

4.1 UTANGULIZI ........ 18
4.2 MAJUMUISHO ........ 18
4.3 HITIMISHO ........ 19

**REJEA** ........ 20

SURA YA KWANZA

# MWELEKEO WA ELIMU JUMUISHI NCHINI

## 1.1 Utangulizi

Sura hii inaeleza kwa ujumla mwelekeo wa elimu jumuishi nchini. Hivyo imeelezea usuli pamoja na umuhimu wa Mwongozo kwa watumiaji wote kuanzia ngazi ya Taifa hadi shule. Pia, imeonyesha malengo mahususi kwa watumiaji wote wa Mwongozo kwa kuzingatia mustakabali wa changamoto mbalimbali zinazoikabili sekta ya elimu ikiwemo ujumuishaji wa watoto wenye mahitaji maalumu. Pamoja na mafanikio katika kutekeleza utoaji wa elimu nchini, Serikali imeandaa Mkakati wa kitaifa unaotoa dira ya utekelezaji wa elimu jumuishi. Hivyo, Mwongozo huu unalenga kutoa maelekezo ya utekelezaji wa Mkakati katika kutambua na kutatua changamoto za ujifunzaji na kutoa afua stahiki kwa wanafunzi katika ngazi ya elimumsingi na sekondari.

## 1.2 Usuli

Tanzania imesaini mikataba mbalimali ya kimataifa na kikanda inayohusu elimu jumuishi. Miongoni mwa mikataba hiyo ni Tamko la Salamanka la 1994 na Tamko la Dakar la 2000 ambayo yameelekeza kila nchi kutafsiri na kutekeleza elimu jumuishi katika mazingira yake. Vilevile, lengo Namba 4 la Malengo Endelevu ya Milenia ya Mwaka 2030 linaweka msisitizo wa utoaji wa elimu kwa usawa na hivyo kuchagiza utekelezaji wa elimu jumuishi nchini. Katika kutekeleza azma ya upatikanaji wa elimu kwa wote, Tanzania imekua ikiandaa mikakati mbalimbali ya utekelezaji wa elimu jumuishi ambayo ni pamoja na ule wa mwaka 2009-2017, 2018-2021 na 2022-2026. Hata hivyo katika kutekeleza mikakati hiyo, OR-TAMISEMI imebaini utofauti mkubwa wa utekelezaji wa elimu jumuishi kati ya shule moja na shule nyingine nchini. Hivyo, OR-TAMISEMI imeandaa Mwongozo huu ili kuwasaidia watekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Elimu Jumuishi wa 2022-2026 waweze kufanikisha utoaji wa elimu katika mazingira jumuishi.

## 1.3 Malengo ya Mwongozo

Mwongozo huu unalenga kuweka taratibu za utekelezaji wa elimu jumuishi katika ngazi mbalimbali kama ifuatavyo:

a) Kutoa maelekezo mbalimbali kwa wasimamizi na watekelezaji

wa elimu jumuishi

b) Kutoa fursa kwa wadau mbalimbali kushirikiana na serikali katika kutekeleza utoaji wa elimu katika mazingira jumuishi
c) Kuongeza uwajibikaji kwenye ngazi mbalimbali zinazohusika na utekelezaji wa elimu jumuishi nchini

### 1.4 Umuhimu wa Mwongozo

Mwongozo huu una umuhimu kama ifuatavyo:

(a) Kuweka mfumo elekezi ya usimamizi wa utekelezaji wa shughuli zote za elimu jumuishi.
(b) Kurahisisha uwajibikaji katika kila ngazi ya kimamlaka bila kuleta mkanganyiko wa kiusimamizi.
(c) Kumsaidia mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu kushiriki ipasavyo kwenye ujifunzaji katika mazingira jumuishi.

### 1.5 Matarajio ya mwongozo

a) Kuimarika kwa utoaji na upatikanaji wa elimu bora kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu
b) Kuboreshwa kwa uratibu na usimamizi wa elimu jumuishi katika ngazi mbalimbali za utawala
c) Kuimarika kwa ujumuishi ndani ya shule na jamii
d) Jamii kushiriki katika utekelezaji wa shughuli za elimu jumuishi

### 1.6 Hitimisho


Watoto wenye mahitaji maalumu wamekuwa na changamoto katika ujifunzaji kwenye mfumo wa elimu nchini. Kwa kutambua hali hiyo, Serikali imeandaa Mwongozo huu ili kuweka utaratibu mzuri wa usimamizi na utekelezaji wa mkakati wa Taifa wa Elimu Jumuishi wa 2022-2026 ambao unatoa utaratibu kwa kila mdau anayehusika katika usimamizi na utekelezaji wa elimu jumuishi katika elimumsingi. Ni matumaini ya serikali kuwa, wadau waliotajwa katika Mwongozo huu watatimiza wajibu wao ili malengo ya Serikali ya kufanikisha utoaji wa elimu jumuishi bora pamoja na ujenzi wa utamaduni jumuishi ndani na nje ya shule yatimie.

SURA YA PILI

# DHANA YA ELIMU JUMUISHI

## 2.1 Utangulizi

Sura hii inaeleza maana, chimbuko, na hali ya elimu jumuishi kwa muktadha wa Tanzania. Hivyo Mwongozo huu unabainisha umuhimu wa elimu jumuishi, makundi stahiki ya wanafunzi, na namna ya utekelezaji wake nchini. Mchoro Na. 1 unaeleza dhana ya utofauti wa mahitaji ya ujifunzaji darasani.




*Mchoro 1: Dhana ya ujumuishi*

## 2.2 Maana ya Elimu Jumuishi

Kumekuwa na tafsiri mbalimbali za elimu jumuishi kutoka nchi moja kwenda nchi nyingine. Kwa muktadha wa Tanzania, Elimu Jumuishi ni mfumo wa utoaji wa elimu kwa wanafunzi wote kwa kuzingatia tofauti zao za ujifunzaji (JMT, 2022). Aidha, ni mchakato wa kuongeza **ushirikishwaji** wa wanafunzi wote shuleni ikiwa ni pamoja na wenye mahitaji maalumu. Mchakato huu ni endelevu unaohusisha kubadili mila, desturi, fikra, imani, mitazamo, sera, mbinu na mazingira ya ujifunzaji. Ili kuongeza ushirikishwaji na kuleta **ufanisi** katika mjumuisho huo, elimu jumuishi inazingatia misingi yake kama ilivyotajwa katika sehemu ifuatayo.

## 2.3 Misingi ya Elimu Jumuishi

Msingi mkuu wa elimu jumuishi ni utoaji wa haki ya elimu kwa kila mtoto, mwenye na asiye na ulemavu. Hivyo, msingi huu unatambua

kwamba:


i. Kila mwanafunzi ana uwezo wa kujifunza
ii. Kila mwanafunzi ana namna mbalimbali za kujifunza na kujieleza
iii. Kila mwanafunzi ana haki ya kushiriki katika zoezi la ujifunzaji
iv. Mwalimu bora ni yule mwenye uwezo na ujuzi wa kutumia mbinu mbalimbali za ufundishaji na ushirikishaji wa wanafunzi
v. Elimu bora ni ile inayozingatia mahitaji ya ujifunzaji ya kila mwanafunzi
vi. Elimu bora ni mfumo nyumbufu

## 2.4 Chimbuko la elimu jumuishi nchini Tanzania

Elimu jumuishi imeanza kutekelezwa siku nyingi nchini Tanzania kupitia Sheria ya Elimu ya 1978 iliyoelekeza upatikanaji wa elimu kwa kila mtoto. Utekelezaji wa sheria hii kwa watoto wenye mahitaji maalumu umerasimishwa mwaka 1998 kupitia mradi wa Wizara ya Elimu kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO). Mradi huo ulitambulika kama ***Special Needs in the Classroom,*** na ulifanyika katika shule za mkoa wa Dar es Salaam. Pamoja na mambo mengine, mradi huu ulifundisha walimu na wazazi umuhimu na namna ya kutekeleza elimu jumuishi. Moja ya matokeo ya mradi huu ni kuandaliwa kwa Mkakati wa 2009/2017. Hata hivyo, Serikali imeendelea kuboresha na kuandaa mikakati ya Taifa ya Elimu Jumuishi ikiwa ni pamoja na wa 2022-2026 ambao ndio msingi wa Mwongozo huu. Ikumbukwe pia kwamba, Tanzania imeridhia mikataba mbalimbali ya kimataifa na kikanda inayoelekeza utoaji wa elimu katika mazingiza jumuishi shuleni. Baadhi ya mikataba hiyo ni ule wa Salamanka wa mwaka 1994 na ule wa Dakar wa mwaka 2000. Hata hivyo, Malengo Endelevu ya Milenia ya 2030 yanatoa dira ya usawa wa elimu kwa makundi yote bila ubaguzi na hii imekuwa chachu kubwa kwa Tanzania kutekeleza maagizo ya mikataba hiyo.

## 2.5 Makundi stahiki ya elimu jumuishi

Mwongozo huu unaainisha makundi mbalimbali ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu kama yalivyoainishwa na Mkakati wa Taifa wa Elimu Jumuishi 2022/26. Baadhi ya makundi hayo ni kama yalivyoainishwa kwenye mchoro ufuatao:





*Mchoro 2: Baadhi ya makundi ya watu wenye mahitaji maalumu*

Kwa minajili ya utoaji wa elimu katika mazingira jumuishi nchini, mwalimu anapaswa kutambua kuwa kuna zaidi ya makundi 17 ya watu wenye mahitahi maalumu ambao wanahitaji umakini katika kuelimishwa. Aina hizi zinatokana na zana zilizotumika katika kubainisha makundi hayo. Kwa mantiki hii, ni wajibu wa kila mwalimu kufahamu mahitaji ya mwanafunzi ya ujifunzaji ili kumpatia afua stahiki kama inavyoelekezwa katika Mwongozo huu.

## 2.6 Changamoto za utekelezaji wa elimu jumuishi

Pamoja na umuhimu wa elimu jumuishi, utekelezaji wake nchini umekuwa ukikabiliwa na changamoto mbalimbali za Ki-sera na kiutendaji. Baadhi ya changamoto hizo ni kama zilivyoainishwa na Mchoro Na. 3 hapo chini. Changamoto hizo zimepelekea kukosekana kwa ufanisi katika ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi wenye mahitaji maalumu – hususani wale wenye uelemavu. Hii imesababisha wengi wao kushindwa kumaliza shule na/ama kufanya vibaya katika masomo na mitihani yao. Aidha, kukithiri kwa mitazamo hasi na mila potofu kwa kundi hili kumesabaisha walimu na wazazi kutowapatia umakini wanafunzi husika kwenye ujifunzaji na baadhi ya wazazi kutowapeleka watoto wao shule (JMT, 2021). Tafiti za hivi karibuni zimebainisha kuwa watoto wengi wenye mahitahi maalumu wamethiriwa, kwa asilimia kubwa, na tamaduni hasi kati ya walimu na wanafunzi; na tamaduni hizo zimeathiri pia tamaduni za shule (Mkama, 2021). Matokeo yake,

shule jumuishi zimekosa tamaduni jumuishi na hivyo kuendeleza uendeshaji wa shule hizo kwa kuzingatia mazoea. Kama ilivyoelekezwa kwenye Mwongozo huu, utekelezaji wa elimu jumuishi nchini unalenga kuondoa mazoea katika uendeshaji wa shule jumuishi na hivyo kuleta ufanisi kwenye elimu kwa makundi yote.




*Mchoro 3: Baadhi ya changamoto za utoaji wa elimu katika mazingira jumuishi*

## 2.7 Hitimisho

Sura hii imeeleza chimbuko la elimu jumuishi nchini na imeainisha dhana, misingi, na makundi ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Aidha, imesisitiza umuhimu wa kuzingatia haki za binadamu katika utoaji wa elimu kwa wanafunzi wote wakiwemo wenye mahitaji maalumu. Ni matarajio ya OR-TAMISEMI kuona kwamba kila mtekelezaji wa Mwongozo huu anakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu dhana ya elimu jumuishi ili kuleta ufanisi katika ujifunzaji kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

SURA YA TATU

# MAENEO YA UTEKELEZAJI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inalenga kuainisha maeneo mbalimbali ya utekelezaji kama yalivyobainishwa kwenye Mkakati wa Taifa wa Elimu Jumuishi wa 2022-2026. Katika kuleta ufanisi wa utekelezaji wa maeneo kusudiwa, sura hii imetafsiri na kuainisha majukumu mbalimbali ya utekelezaji wa elimu jumuishi katika maeneo mahususi ya ki-sera na utoaji wa elimu katika mazingira jumuishi. Hivyo katika kutekeleza maelekezo ya sura hii, unahitajika kusoma kwa makini na kuelewa eneo husika la utekelezaji kama ilivyoelezwa hapa chini:

## 3.2 Maeneo ya Utekelezaji

### 3.2.1 Kutafsiri kwa vitendo Sera, Sheria, Miongozo, Nyaraka na Matamko ya elimu ili kutekeleza elimu jumuishi nchini

Eneo hili la utekelezaji linalenga kuboresha, kuimarisha na kuhawilisha uelewa na utekelezaji wa sera, miongozo, nyaraka na matamko yote yanayohusu utoaji wa elimu katika mifumo jumuishi kuanzia ngazi ya taifa mpaka shule. Ili kufikia lengo hili, Mwongozo huu unaelekeza kufanyika kwa mambo yafuatayo:

i. Kuhawilisha na kusambaza miongozo mbalimbali katika ngazi zote ili kuleta uelewa wa pamoja wa dhana na malengo ya elimu jumuishi nchini
ii. Kuanzisha na kusimamia vitengo vya ushauri na unasihi ili kutoa afua stahiki kwa wanafunzi wenye na wasio na mahitaji maalumu
iii. Kuanzisha na kusimamia mifumo ya utoaji na upatikanaji wa taarifa inayofikika kwa urahisi shuleni na ofisini
iv. Kuwajengea uwezo watumishi juu ya uelewa, usimamizi na utekelezaji wa elimu jumuishi
v. Kutoa fursa kwa wasaidizi wa walimu katika madarasa jumuishi kupitia ofisi ya mkurugenzi wa halmashauri
vi. Kutoa fursa kwa walimu wa kujitolea hasa kwenye fani ya elimu maalumu na/au jumuishi

### Viashiria vya Utekelezaji

Ili kubaini kiwango cha utekelezaji wa shughuli zilizoainishwa chini ya eneo hili la utekelezaji, Mwongozo unatoa viashiria vitakavyo

onyesha utekelezaji huo. Hivyo wafuatiliaji wote wanatakiwa kuzingatia viashiria hivyo kama ifuatavyo:

i. Uwepo kwa vitengo vya unasihi kwa kila shule
ii. Uwepo wa mifumo ya wazi ya kutolea taarifa mfano muhtsari ya vikao, ratiba ya vikao, na mbao za matangazo
iii. Uwepo wa mpango kazi na taarifa za mafunzo, vikao kazi, warsha na makongamano yanayohusu elimu jumuishi
iv. Uwepo wa sera, miongozo na mikakati katika ngazi zote za kielimu
v. Ongezeko la wataalumu wa elimu jumuishi katika ngazi mbalimbali
vi. Uwepo wa wasaidizi wa walimu katika ngazi ya shule
vii. Uwepo wa walimu wa kujitolea shuleni

## Majukumu

Katika kutekeleza malengo ya eneo hili la utendaji, OR-TAMISEMI katika ngazi mbaimbali za kiutendaji ina majukumu mbalimbali ambayo yanatekelezwa kwa kuzingatia hati ya ugatuaji wa madaraka wa 2013. Hivyo, Mwongozo huu unaainisha majukumu ya ofisi mbalimbali za kama ifuatavyo:

### 3.2.1.1 Ofisi ya Rais TAMISEMI

Ili kuhahakisha uboreshaji, uimarishaji, uhawilishaji na utekelezaji wa sera, miongozo, nyaraka na matamko yote yanayohusu elimu unafanyika katika mifumo jumuishi, OR-TAMISEMI ina majukumu yafuatayo:

i. Kuanzisha, kusimamia na kuboresha vitengo vya ushauri na unasihi
ii. Kuanzisha na kusimamia mifumo ya utoaji na upatikanaji wa taarifa inayofikika kwa urahisi shuleni na ofisini
iii. Kuwajengea uwezo watumishi juu ya uelewa, usimamizi na utekelezaji wa elimu jumuishi
iv. Kuhawilisha na kusambaza miongozo mbalimbali katika ngazi zote
v. Kutoa fursa za wasaidizi wa walimu kwa madarasa jumuishi kupitia ofisi ya mkurugenzi wa halmashauri
vi. Kutoa fursa kwa walimu wa kujitolea

### 3.2.1.2 Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa

Katika kufanikisha malengo ya kutafsiri kwa vitendo Sera, Sheria, Miongozo, Nyaraka na Matamko ya elimu jumuishi nchini, ofisi ya

katibu tawala mkoa na idara za kisekta zina majukumu ya kufuatilia yafuatayo:

i. Kuanzisha, kusimamia na kuboresha vitengo vya ushauri na unasihi
ii. Kuanzisha na kusimamia mifumo ya utoaji na upatikanaji wa taarifa inayofikika kwa urahisi shuleni na ofisini
iii. Kuwajengea uwezo watumishi juu ya uelewa, usimamizi na utekelezaji wa elimu jumuishi
iv. Kuhawilisha na kusambaza miongozo mbalimbali katika ngazi zote
v. Kutoa fursa za wasaidizi wa walimu katika madarasa jumuishi kupitia ofisi ya mkurugenzi wa halmashauri
vi. Kutoa fursa kwa walimu wa kujitolea

### 3.2.1.3 Mkurugenzi wa Halmshauri

Katika kufanikisha malengo ya eneo hili la utekelezaji, Mkurugenzi wa halmashauri ana majukumu yafuatayo:

i. Kuanzisha, kusimamia na kuboresha vitengo vya ushauri na unasihi
ii. Kuanzisha na kusimamia mifumo ya utoaji na upatikanaji wa taarifa inayofikika kwa urahisi shuleni na ofisini
iii. Kuwajengea uwezo watumishi juu ya uelewa, usimamizi na utekelezaji wa elimu jumuishi
iv. Kuhawilisha na kusambaza miongozo mbalimbali katika ngazi zote
v. Kutoa fursa za wasaidizi wa walimu katika madarasa jumuishi kupitia ofisi ya mkurugenzi wa halmashauri
vi. Kutoa fursa kwa walimu wa kujitolea

### 3.2.1.4 Ofisi ya Kata

Katika kufanikisha malengo ya eneo hili la utekelezaji, ofisi ya Afisa Elimu Kata ina majukumu ya kuratibu mambo mbalimbali ikiwemo:

i. Uanzishwaji na uboreshaji wa vitengo vya ushauri na unasihi
ii. Kuwajengea uwezo watumishi juu ya uelewa, usimamizi na utekelezaji wa elimu jumuishi
iii. Uanzishwaji mifumo ya utoaji na upatikanaji wa taarifa inayofikika kwa urahisi shuleni na ofisini
iv. Usambazaji miongozo mbalimbali

#### 3.2.1.5 Shule

##### 3.2.1.5.1 Kamati na Bodi za Shule

i. Kuanzisha na kusimamia vitengo vya ushauri na unasihi
ii. Kusimamia mifumo ya utoaji na upatikanaji wa taarifa inayofikika kwa urahisi shuleni
iii. Kuhamasisha umuhimu wa utekelezaji wa elimu jumuishi
iv. Kufanya tathmini ya utekezaji wa elimu jumuishi
v. Kutoa fursa za wasaidizi wa walimu kwa madarasa jumuishi
vi. Kutoa fursa kwa walimu wa kujitolea

##### 3.2.1.5.2 Mkuu wa Shule

i. Kuanzisha na kusimamia vitengo vya ushauri na unasihi
ii. Kuanzisha na kusimamia mifumo ya utoaji na upatikanaji wa taarifa inayofikika kwa urahisi shuleni na ofisini
iii. Kuwajengea uwezo watumishi juu ya uelewa, usimamizi na utekelezaji wa elimu jumuishi
iv. Kuhawilisha na kusambaza miongozo mbalimbali katika ngazi zote
v. Kutoa fursa za wasaidizi wa walimu kwa madarasa jumuishi kupitia ofisi ya Mkurugenzi wa halmashauri
vi. Kutoa fursa kwa walimu wa kujitolea hasa wenye fani stahili za elimu maalumu/jumuishi

##### 3.2.1.5.3 Mwalimu

i. Kutoa huduma ya ushauri na unasihi kwa kufuata miongozo
ii. Kuandaa taarifa kulingana na mahitaji ya mifumo

### 3.2.2 Utoaji wa elimu katika mazingira jumuishi

Eneo hili la utekelezaji linalenga kuboresha upatikanaji wa elimu katika mazingira jumuishi kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Pia, linasisitiza kuimarishwa kwa **ushirikishwaji** wa wanafunzi hao katika ujifunzaji. Ili kufikia malengo haya, Mwongozo huu unaelekeza kufanyika kwa mambo yafuatayo:

i. Uanzishaji wa vituo vya upimaji wa kubaini mahitaji maalumu ya kielimu katika halmashauri
ii. Kufanyika kwa zoezi endelevu la ubainishaji na utambuzi wa watoto wenye mahitaji maalumu ndani na nje ya shule
iii. Upimaji wa watoto ili kubaini wenye mahitaji maalumu kwa ajili ya ujifunzaji bora kwa kuzingatia mwongozo husika

iv. Kuandikisha na kusajili watoto wenye mahitaji maalumu katika mifumo rasmi
v. Uwezeshaji na ufuatilia wa utekelezaji wa elimu jumuishi kwa walimu
vi. Uandaaji na utekelezaji wa mpango binafsi wa ujifunzaji (*Individualized Education Program [IEP]*[1])
vii. Uanzishwaji wa ufundishaji shirikishi (*collaborative teaching*) kati ya mwalimu na msaidizi wa mwalimu darasani nan je ya darasa
viii. Utumiaji wa mbinu mbalimbali za ujifunzaji na za kujieleza ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu
ix. Uanzishaji na utekelezaji wa utamaduni jumuishi kwa kuzingatia mazingira halisi ya shule
x. Kusambaza, kufuatilia na kukarabati vifaa maalumu na vifaa saidizi vya kufundishia na kujifunzia kulingana na mwongozo husika
xi. Ushiriki wa wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika shughuli mbalimbali za ndani na nje ya darasa
xii. Uratibu na ufuatiliaji wa shughuli za elimu jumuishi zinazotekelezwa na wadau mbalimbali
xiii. Uanzishwaji ya mabweni shuleni ili kupunguza uwezekano wa madhara kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu
xiv. Kunyumbua programu za shule ili kuweka muda wa kutosha wa wanafunzi kujifunza stadi za maisha – hasa kwa wanafunzi wenye ulemavu

## Viashiria vya utekelezaji

Ili kubaini kiwango cha utekelezaji wa shughuli zilizoainishwa chini ya eneo hili la utekelezaji, Mwongozo huu unatoa viashiria vitakavyoonesha utekelezaji wake. Hivyo, watekelezaji wa Mwongozo huu wanatakiwa kuzingatia viashiria vifuatavyo:

i. Uwepo wa vituo vya upimaji
ii. Uwepo wa taarifa za watoto waliobainishwa
iii. Uwepo wa taarifa ya watoto waliofanyiwa upimaji wa kubaini mahitaji maalumu ya ujifunzaji
iv. Uwepo wa watoto wenye mahitaji maalumu waliojumuishwa kwenye mfumo wa elimu
v. Uwepo wa utamaduni na madarasa jumuishi
vi. Uwepo wa taarifa za mafunzo juu ya elimu jumuishi
vii. Uwepo wa mpango binafsi wa ujifunzaji (*Individualized Education Program [IEP]*)
viii. Uwepo wa vifaa maalumu na vifaa saidizi vinavyotumika kama ilivyokusudiwa
ix. Uwepo wa michezo mbalimbali inayowahusisha wanafunzi wenye mahitaji maalumu
x. Uwepo wa taarifa zinazotokana na ushiriki wa wadau mbalimbali
xi. Uwepo wa mabweni yenye wanafunzi wenye mahitaji maalumu

1 Angalia kiambatisho A

xii. Uwepo wa programu zinazokuza stadi za maisha kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu – hasa wale wenye ulemavu

## Majukumu

Katika kutekeleza malengo ya eneo hili la utendaji, Mwongozo huu unaainisha majukumu ya ofisi mbalimbali za kama ifuatavyo:

### 3.2.2.1 Ofisi ya Rais TAMISEMI

Ili kuhahakisha kwamba kuna utoaji wa elimu katika mazingira jumuishi, OR-TAMISEMI ina majukumu yafuatayo:

i. Kuandaa, kusambaza na kusimamia miongozo ya utekelezaji wa uanzishaji na uendeshaji wa vituo vya upimaji wa kubaini mahitaji maalumu ya kielimu katika halmashauri
ii. Kufuatilia utekelezaji wa shughuli za ubainishaji, utambuzi na upimaji wa watoto wenye mahitaji maalumu
iii. Kuratibu uandikishaji na usajili wa watoto wenye mahitaji maalumu katika mifumo rasmi
iv. Kusimamia utekelezaji wa elimu jumuishi
v. Kusimamia ujenzi na uboreshaji wa miundombinu rafiki kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu
vi. Kusimamia usambazaji na ukarabati wa vifaa maalumu na vifaa saidizi
vii. Kusimamia ushiriki wa wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika michezo mbalimbali
viii. Kuratibu na kufuatilia shughuli za elimu jumuishi zinazotekelezwa na wadau mbalimbali
ix. Kuratibu na kufuatilia programu za shule na kuhakikisha zinatenga muda wa kukuza stadi za maisha kwa wanafunzi
x. Kuratibu na kufuatilia uanzishwaji wa mabweni shuleni

### 3.2.2.2 Ofisi ya katibu Tawala wa Mkoa

Katika kufanikisha malengo ya utoaji wa elimu katika mazingira jumuishi, ofisi ya katibu tawala mkoa na idara za kisekta zina majukumu ya kufuatilia yafuatayo:

i. Uanzishwaji na uendeshaji wa vituo vya upimaji wa kubaini mahitaji maalumu ya kielimu
ii. Utekelezaji wa ubainishaji, utambuzi na upimaji wa watoto wenye mahitaji maalumu ndani na nje ya shule
iii. Uandikishaji na usajili wa watoto wenye mahitaji maalumu katika mifumo rasmi
iv. Utekelezaji wa elimu jumuishi
v. Uanzishaji na utekelezaji wa utamaduni jumuishi
vi. Usambazaji na ukarabati vifaa maalumu na vifaa saidizi

vii. Ushiriki wa wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika michezo mbalimbali
viii. Kuratibu shughuli za elimu jumuishi zinazotekelezwa na wadau mbalimbali
ix. Kuratibu uanzishwaji wa mabweni shuleni kulingana na mahitaji

### 3.2.2.3 Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri

Katika kufanikisha utoaji wa elimu katika mazingira jumuishi, ofisi ya mkurugenzi wa halmashauri ina majukumu yafuatayo:

i. Kuratibu uanzishaji na uendeshaji wa vituo vya upimaji wa kubaini mahitaji maalumu
ii. Kusimamia utekelezaji wa ubainishaji, utambuzi na upimaji wa watoto wenye mahitaji maalumu ndani na nje ya shule
iii. Kusimamia uandikishaji na usajili wa watoto wenye mahitaji maalumu katika mifumo rasmi
iv. Kufuatilia utekelezaji wa elimu jumuishi
v. Kusimamia uanzishaji na utekelezaji wa utamaduni jumuishi
vi. Kuratibu usambazaji, ufuatiliaji na ukarabati wa vifaa maalumu na vifaa saidizi
vii. Kuratibu ujenzi na uboreshaji wa miundombinu rafiki kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu
viii. Kuratibu upatikanaji wa taarifa sahihi za wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika mfumo wa utahini
ix. Kuratibu ushiriki wa wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika michezo mbalimbali
x. Kuratibu ujenzi wa mabweni shuleni kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu
xi. Kuratibu usafiri wa wanafunzi wenye ulemavu walioko bweni kwa kuwapeleka shule na kuwarudisha nyumbani wakati wa likizo
xii. Kusimamia ruzuku ya chakula kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu
xv. Kusimamia shughuli za elimu jumuishi zinazotekelezwa na wadau mbalimbali
xvi. Kuratibu mafunzo kazini kwa walimu ili kutekelekeza elimu jumuishi

### 3.2.2.4 Ofisi ya Kata

Katika kufanikisha malengo utoaji wa elimu katika mazingira jumuishi, ofisi ya Afisa Elimu Kata ina majukumu ya kuratibu yafuatayo:

i. Mchakato wa ubainishaji, utambuzi na upimaji wa watoto wenye mahitaji maalumu
ii. Uandikishaji na usajili wa watoto wenye mahitaji maalumu katika mifumo rasmi
iii. Utekelezaji wa elimu jumuishi

iv. Uanzishaji na utekelezaji wa utamaduni jumuishi
v. Usambazaji na ukarabati vifaa maalumu na vifaa saidizi
vi. Upatikanaji wa taarifa sahihi za wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika mfumo wa utahini
vii. Upatikanaji wa mabweni kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu
viii. Ushiriki wa wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika michezo mbalimbali
ix. Matumizi ya ruzuku ya chakula kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu
x. Shughuli za elimu jumuishi zinazotekelezwa na wadau mbalimbali
xi. Mpango kazi wa mafunzo ya walimu kazini ili kutekeleza elimu jumuishi

#### 3.2.2.5 Shule

##### 3.2.2.5.1 Kamati na Bodi za Shule

Katika kufanikisha utoaji wa elimu katika mazingira jumuishi, kamati na bodi ya shule zina majukumu yafuatayo:

i. Kushiriki katika uhamasishaji wa ubainishaji, utambuzi na upimaji wa watoto wenye mahitaji maalumu
ii. Kushiriki katika uhamasishaji wa uandikishaji wa watoto wenye mahitaji maalumu
iii. Kusimamia utekelezaji wa utamaduni na elimu jumuishi shuleni
iv. Kupokea na kusimamia utumiaji na ukarabati wa vifaa maalumu na vifaa saidizi
v. Kusimamia upatikanaji wa taarifa sahihi za wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika mfumo rasmi
vi. Kuhamasisha na kusimamia wadau katika utekelezaji wa elimu jumuishi
vii. Kusimamia ujenzi na uboreshaji wa miundombinu rafiki kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu
viii. Kusimamia ujenzi wa mabweni kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu
ix. Kusimamia ushiriki wa wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika michezo mbalimbali
x. Kusimamia ruzuku ya chakula kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu
xi. Kusimamia mpango wa mafunzo ya walimu kazini ili kutekeleza elimu jumuishi

##### 3.2.2.5.2 Mkuu wa Shule

Katika kufanikisha utoaji wa elimu katika mazingira jumuishi, mkuu wa

shule ana majukumu yafuatayo:

i. Kusimamia utekelezaji wa ubainishaji, utambuzi na upimaji wa watoto wenye mahitaji maalumu ndani ya shule
ii. Kuandikisha na kusajili watoto wenye mahitaji maalumu katika mifumo rasmi
iii. Kusimamia utekelezaji wa elimu jumuishi kwa kuhakikisha kila mwanafunzi anapata nafasi ya kujifunza ndani na nje ya darasa bila ubaguzi wowote
iv. Kusimamia utekelezaji wa ufundishaji shirikishi (*collaborative teaching*) darasani/shuleni
v. Kusimamia uboreshaji wa programu za shule ili kutoa muda wa wanafunzi kujifunza na kukuza stadi za maisha
vi. Kusimamia uandaaji, utekelezaji na ufuatiliaji wa mpango binafsi wa ujifunzaji kwa wanafunzi (*Individualized Education Program [IEP]*)
vii. Kusimamia uandaaji na utumiaji mbinu za ufundishaji zitakazokidhi utekelezaji wa elimu jumuishi
viii. Kusimamia uanzishaji na utekelezaji wa utamaduni jumuishi shuleni
ix. Kufuatilia upatikanaji wa vifaa maalumu na vifaa saidizi ili kuhakikisha mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu anapata huduma stahiki kwa wakati
x. Kupokea na kusimamia matumizi sahihi ya vifaa maalumu na vifaa saidizi
xi. Kutoa taarifa sahihi za wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika mfumo wa utahini
xii. Kuratibu ujenzi na uboreshaji wa miundombinu rafiki kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu
xiii. Kuratibu ujenzi wa mabweni kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu
xiv. Kusimamia ushiriki wa wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika michezo mbalimbali
xv. Kusimamia upatikanaji na matumizi ya ruzuku ya chakula kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu
xvi. Kushirikiana na wadau katika kutekeleza shughuli za elimu jumuishi
xii. Kuandaa mpango wa mafunzo ya walimu kazini ili kutekeleza elimu jumuishi
xiii. Kuratibu uwepo wa chumba maalumu cha ujifunzaji (*Resource Room*) ambacho kitatumika kuhifanidhia zana na vifaa vya ujifunzaji na ambacho kinaweza kutumiwa kwa ujifunzaji wa ziada kwa wale wenye mahitaji maalumu.

### 3.2.2.5.3 Mwalimu

Katika kufanikisha malengo utoaji wa elimu katika mazingira jumuishi,

mwalimu anapaswa kutekeleza yafuatayo:

i. Kutambua kwamba kila mwanafunzi ana uwezo wa kujifunza na hivyo kumpa kila mwanafunzi nafasi ya kuchangia kwenye ujifunzaji
ii. Kuwezesha ujifunzaji na ufundishaji unaojenga umahiri katika kumudu stadi mbalimbali za maisha
iii. Kutumia mbinu mbalimbali za uwasilishaji na ushirikishaji wa wanafunzi: Mwalimu anapaswa kutambua kwamba wanafunzi wote hawana ufanano katika ujifunzaji. Wapo wanaojifunza kwa kutazama picha, kwa kusikiza, kwa kujadili kwenye makundi, kwa kusoma peke yao, wengine wanahitaji maelezo ya kujirudia na wengine usimamizi wa karibu
iv. Kuwapatia wanafunzi namna tofauti za kujifunza na kujieleza kwa kuzingatia utofauti wao wa mawasiliano: mwalimu awaruhusu wanafunzi wajieleze kwa kuchora, kutumia lugha ya alama, kuzungumza, na kuandika
v. Kuwa makini na chochote kitakachoharibu ujifunzaji wa wanafunzi (*proactive*) darasani na kukizuia: mwalimu kuwa mvumilivu kwa wanafunzi na kuwafundisha kwa upendo na kukuza mahusiano chanya baina ya wanafunzi
vi. Kutengeneza mazingira jumuishi ambayo ni rafiki na nyumbufu darasani ili kupanua uwigo wa upatikanaji wa elimu kwa wanafunzi wote
vii. Kutoa fursa kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu – hususani wenye ulemavu – kuchangia katika ujifunzaji darasani na nje ya darasa
viii. Kutumia mbinu ya **ufundishaji shirikishi** (*collaborative teaching*) kati yake na msaidizi wake. Katika ufundishaji huu, msaidizi wa mwalimu atafundisha kile ambacho mwalimu atamuelekeza kufanya
ix. Kutumia mbinu ya **kushirikishana** katika ufundishaji (*team-teaching*) kati ya walimu wawili au zaidi katika kupanga, kufundisha na kutathimini ujifunzaji
x. Kusisitiza mbinu ya ujifunzaji ya **Mwanafunzi-kwa-Mwanafunzi** (*Peer-to-Peer tutoring*) kwenye ujifunzaji – ndani na nje ya darasa kwa kuhimiza wanafunzi walio na uwezo kusoma na wenzao katika vikundi ili kusaidiana. Njia hii pia inasaidia kwa wanafunzi wenye na wasio na ulemavu kusaidiana.
xi. Kushirikiana na wadau katika kuandaa na kutekeleza mpango binafsi wa ujifunzaji (*Individualized Education Program [IEP]*) hasa kwa wanafunzi wanaohitaji muda wa ziada wa kujifunza
xii. Kushiriki katika kujenga utamaduni jumuishi shuleni kwa mfano; kuanzisha vilabu na vikundi vya kuhamasisha ujumuishi
xiii. Kuwashirikisha wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika michezo mbalimbali ili kuwakuzia vipawa katika ujifunzaji wao
xiv. Kutunza, kutumia na kutoa taarifa za uchakavu wa vifaa maalumu

na vifaa saidizi

xv. Kushirikiana na wadau katika kutekeleza shughuli za elimu jumuishi

xvi. Kuhakikisha zana zote za ufundishaji zinabandikwa ukutani au kuwekwa mahali pa wazi ili wanafunzi wajifunze zaidi baada ya darasani

#### 3.2.2.5.4 Msaidizi wa Mwalimu

Katika kutekeleza utoaji wa elimu katika mazingira jumuishi, kutakuwa na msaidizi wa mwalimu ambaye anaweza kuwa ni mzazi, mwalimu, mwanafunzi au mtaalamu yoyote wa elimu maalumu ambaye atakua na majukumu mbalimbali ikiwa ni pamoja na:

i. Kumsaidia mwanafunzi mmoja mmoja au darasa kwa ujumla kulingana na mahitaji ya ujifunzaji

ii. Kumsaidia mwalimu wa somo katika kusimamia shughuli za ujifunzaji kulingana na melekezo ya mwalimu

iii. Kushiriki katika kuaanda na kutekeleza wa mpango binafsi wa ujifunzaji wa mwanafunzi

iv. Kuwa kiungo cha mawasiliano kati ya shule na mzazi

v. Kumhamasisha mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu kushiriki katika ujifunzaji

### 3.3 Hitimisho

Utoaji wa elimu katika mazingira jumuishi na ujenzi wa elimu jumuishi ni zoezi endelevu katika elimu. Ni dhana ambayo kila mdau wa elimu anapaswa kuchangia kwa namna moja ama nyingine na si suala la mwalimu peke yake. Ujumuishi ni dhana inayohimiza **‘umoja kwenye utofauti’** yaani *‘unit in difference’* ambayo ni msingi wa kuheshimu ufofauti wa kila mmoja. Kama ilivyoainishwa kwenye sehemu 2.6 ya Mwongozo huu, utekelezaji wa elimu jumuishi unahitaji dhamira ya dhati. Sura hii imebainisha maeneo yanayopaswa kuzingatiwa katika utekelezaji wa elimu jumuishi nchini. Aidha, imeainisha misingi na majukumu ya utekelezaji katika ngazi mbalimbali ili kuleta ufanisi wa toaji elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Ni matarajio ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI kuwa kila ngazi iliyotajwa katika sura hii ikitekeleza wajibu wake kutakuwa na ufanisi wa utoaji wa elimu katika mazingira jumuishi nchini hivyo kuwawezesha wanafunzi wenye mahitaji maalumu – hususani wenye ulemavu – kupata elimu bora kwa ajili ya maendeleo yao binafsi na ya Taifa kwa ujumla.

SURA YA NNE

# MAJUMUISHO


## 4.1 Utangulizi

Sura hiii inatoa muhtasari wa mada zilizowasilishwa katika Mwongozo huu kwa kuangazia baadhi ya mambo muhimu ambayo mtekelezaji wa Mwongozo anatakiwa kuyazingatia ili kuleta ufanisi. Hivyo, sura imegawanyika katika sehemu tatu ambazo ni utangulizi, majumuisho na hitimisho.

## 4.2 Majumuisho

Ubora na ufanisi wa elimu jumuishi Tanzania unaendelea kuimarika siku hadi siku kutokana na juhudi za Serikali zakutekeleza malengo ya mikataba ya kimataifa, kikanda na kitaifa. Ili kuweza kufanikisha azma ya serikali ya utoaji wa elimu kwa wote, Mwongozo huu unawaelekeza wasimamizi na watekelezaji wa elimu jumuishi kuelewa majukumu yao ili kutekeleza malengo ya Mkakati wa Taifa wa Elimu Jumuishi wa 2022-2026. Mwongozo umetafsiri dhana ya elimu jumuishi katika mazingira ya kitanzania na kuainisha misingi ya utekelezaji wake kwa kuzingatia raslimali zilizopo. Mwongozo huu pia umesisitiza ujenzi wa utamaduni jumuishi ikiwa ni njia ya kuwafanya wanafunzi wenye na wasiokua na mahitaji maalumu kujifunza pamoja bila kujali tofauti zao.

Katika kutatua changamoto za elimu jumuishi nchini na kuleta ufanisi kwenye ujifunzaji wa wanafunzi wenye mahitaji maalumu kwenye mazingira jumuishi, Mwongozo huu umezingatia zaidi mbinu ya Njia Pacha (*Twin-Track Approach)* ambayo inaainisha namna bora ya utatuzi wa changamoto zinazokabili mfumo wa uendeshaji wa elimu katika mazingira jumuishi (Tazama Mchoro Na. 4). Mbinu hii inahakikisha wanafunzi wote wenye mahitaji maalumu – hasa wale wenye ulemavu – wanapata afua stahiki katika mazingira jumuishi ya kujifunzia kwa **kuondoa vikwazo** vya ujifunzaji na **kuongeza upatikanaji** wa huduma stahiki.




*Mchoro 4: Njia Pacha ya utekelezaji wa elimu jumuishi*

Kwa kuzingatia umuhimu wa upatikaji wa elimu katika mziangira jumuishi, uandaaji wa Mwongozo huu umezingatia vipengele vya utekelezaji vilivyoainishwa kwenye Mkakati tajwa. Pia, maelekezo ya Mwongozo huu yamezingatia Miongozo ya OR-TAMISEMI ambayo ni ule wa *Changamoto katika Uboreshaji Elimumsingi na Sekondari: Nini kifanyike* (2022) na *Mkakati wa Kuimarisha Ufundishaji Na Ujifunzaji Ngazi Ya Elimu Msingi* (2022).

## 4.3 Hitimisho

Ofisi ya Rais -TAMISEMI ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa utoaji wa elimu nchini ikiwa ni pamoja na elimu jumuishi. Katika kuhakikisha kwamba kuna usimamizi mzuri na wenye tija, OR-TAMISEMI imeandaa Mwongozo huu ili kutoa dira kwa watekelezaji. Hivyo, kila ngazi na/au ofisi iliyotajwa katika Mwongozo huu ina jukumu la kuusoma kwa kina na kuuelewa ili kutekeleza maelekezo yaliyotolewa.

# REJEA

JMT. (1999). *Dira ya Maendelea ya Taifa 2025*. Dodoma. Wizara ya Fedha na Mipango

JMT. (2005). *Mwongozo wa Ufundishaji Elimu Jumuishi*. Dar es Salaam: Wizara ya Elimu na Ufundi

JMT. (2014). *Sera ya elimu na mfunzo*. Dar Es Salaam: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

JMT. (2021). *Mkakati wa Elimu Jumuishi 2022-2026*. Dodoma. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

JMT. (2022), *Mkakati wa Kuimarisha Ufundishaji Na Ujifunzaji Ngazi Ya Elimu Msingi*. Dodoma: Ofisi ya Rais -TAMISEMI.

JMT. (2022). *Mwongozo wa Uteuzi wa Viongozi wa Elimu Katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mikoa*. Dodoma: Ofisi ya Rais-TAMISEMI.

JMT. (2022). *Changamoto katika Uboreshaji Elimumsingi na Sekondari: Nini Kifanyike?* Dodoma: Ofisi ya Rais-TAMISEMI.

Mkama. I. (2021). *An In-Depth Exploration of the First Phase of Inclusive Deaf Education in Tanzania*. Johannesburg, Universi8ty of the Witwatersrand, South Africa.

Ticha. R; Johnstone. C; Abery. H. B; Pohosyan. A. (2018). *Inclusive Education Strategies: A Textbook*. USA. University of Minosota.

*Kiambatisho A*

**FOMU YA MPANGO BINAFSI WA KIELIMU KWA MWANAFUNZI MWENYE MAHITAJI MAALUMU**

A. **Taarifa Binafsi za Mwanafunzi:**

(i) Jina la Mwanafunzi ______________________________________________
(ii) Jinsi____________________________________________________
(iii) Tarehe ya kuzaliwa____________________________________________
(iv) Hali aliyonayo ______________________________________________
(v) Shule/Kitengo________________________Wilaya____________________
(vi) Mkoa____________________________________________________

B. **Taarifa za wazazi/Walezi**

| Jina | Uhusiano | Kazi | Makazi | Anuani | Simu |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |
| | | | | | |

C. **Changamoto zinazomkabili mwanafunzi**

______________________________________________________________________________
______________________________________________________________________________
______________________________________________________________________________

D. **Uwezo wa Utendaji wa Kielimu kwa mwanafunzi**

| Eneo la Mpango | Hali ya sasa | | Malengo ya muda mfupi | Malengo ya muda mrefu |
|---|---|---|---|---|
| | Anachoweza | Asichoweza | | |
| Uwezo wa kitaaluma;<br>(a) Kusoma<br>(b) Kuandika<br>(c) Kuhesabu | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| Stadi za Kijamii | | | | |
| Stadi za Lugha | | | | |
| Tabia | | | | |
| Stadi za Kujimudu | | | | |
| Maeneo Mengine | | | | |

E. **Utekelezaji wa Mpango**

| Eneo la Mpango | Lengo Mahsusi | Shughuli | Muhusika | Tarehe ya Kuanza | Tarehe ya Kumaliza | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Uwezo wa Kitaaluma | | | | | | |
| Stadi za Kujongea | | | | | | |
| Stadi za Kijamii | | | | | | |
| Stadi za Lugha | | | | | | |
| Tabia | | | | | | |
| Stadi za Kujimudu | | | | | | |
| Maeneo Mengine | | | | | | |

**F. Makubaliano ya Utekelezaji wa Mpango**

| **Mhusika** | | **Jina** | **Saini** |
|---|---|---|---|
| Mzazi/Mlezi | Baba | | |
| | Mama | | |
| | Mlezi | | |
| Mwalimu | | | |
| Wataalamu wengine | | | |
| | | | |
| | | | |

**Tarehe ya kukutana kupanga mpango** ______________________________________

**Mji wa Magufuli - Mtumba**
Mtaa wa TAMISEMI
S.L.P 1923,
41185 Dodoma, Tanzania
**Simu** : (255) 26 232 1 234
**Barua Pepe** : ps@tamisemi.go.tz

**www.tamisemi.go.tz**